Habari

- 26.**-(1) Kutakuwa na Mfuko wa Huduma za Habari.
(2) Mfuko wa Huduma za Habari utaendeshwa na Bodi.
(3) Malengo ya Mfuko wa Huduma za Habari yatakuwa:-
(a) kukuza maudhui ya ndani ya nchi;
(b) kuhimiza weledi katika Tasnia ya Habari; na
(c) kukuza na kuchangia utafiti na maendeleo katika nyanja za habari na Vyombo vya Habari.

Vyanzo vya
Fedha za Mfuko

- 27.** Vyanzo vya Fedha za Mfuko wa Huduma za Habari vitatokana na:
(a) fedha itakayoidhinishwa na Bunge;
(b) misaada, zawadi na michango ya wahisani;
(c) ada inayolipwa kutokana na huduma zinazotolewa na Baraza; na
(d) fedha ambayo kwa namna yoyote italipwa kwa Baraza kwa mujibu wa Sheria hii, au itakayopatikana wakati wa kutekeleza majukumu ya Bodi.

Hesabu na
Ukaguzi wa
Mfuko

- 28.**-(1) Bodi itafungua akaunti kwa ajili ya Mfuko wa Huduma za Habari ambayo itatunza fedha zinazopatikana kwa madhumuni ya Mfuko wa Huduma za Habari.
(2) Bodi itatunza Vitabu vya Hesabu za Mfuko na kumbukumbu nyingine zinazohusiana na hesabu za Mfuko.
(3) Bodi, ndani ya miezi sita baada ya mwaka wa fedha kuisha, itawasilisha kwa Waziri taarifa za fedha zilizokaguliwa.

SEHEMU YA SABA
KASHFA

Kashfa kwa
maneno

- 29.**-(1) Jambo lolote, kama likichapishwa, kutangazwa linaweza kuharibu sifa ya mtu yeyote kwa kumfanya achukiwe, adharauliwe au afanyiwe kejeli au linaloweza kumharibia mtu kazi yake

kwa kuchafua jina lake au kumvunjia heshima yake, jambo hilo litahesabika kuwa ni Kashfa.

(2) Jambo linaloelezwa katika kifungu kidogo cha (1) litakuwa suala la kashfa hata kama limechapishwa au kutangazwa dhidi ya mtu aliyefariki dunia.

(3) Mashtaka ya kashfa yanayomhusu mtu aliyefariki dunia hayawezi kufunguliwa isipokuwa kwa idhini ya Mkurugenzi wa Mashtaka.

(4) Mtu yeyote ambaye kwa kuchapisha, kuandika, kuchora kutumia kinyago au kwa njia nyingine yoyote isipokuwa kwa ishara peke yake, maneno ya mdomo au sauti nyingine kwa makusudi ya kumkashfu mtu huyo, atakuwa ametenda kosa la kashfa.

Kashfa kwa maandishi

30.-(1) Mtu atahesabika kuwa amechapisha suala la kashfa, ikiwa mtu huyo amesababisha kuchapishwa, kuandikwa, kuchorwa, kutengenezwa kinyago au kwa namna nyingine yoyote ambayo suala la kashfa limewasilishwa, limeshughulikiwa kwa maonesho, kusomwa, kunakiliwa, kuelezwa, kupokelewa au vinginevyo, kwa njia ambayo maana ya kashfa itajulikana kwa mtu aliyekashifiwa au mtu mwingine yeyote.

(2) Haitakuwa lazima kwamba uchapishaji au utangazaji wa kashfa umetolewa kwa waziwazi au kikamilifu.

(3) Kwa madhumuni ya kifungu kidogo cha (2), inatosha kama hiyo kashfa inaeleweka kuwa inamhusu huyo mtu aliyekashifiwa kutokana na maelezo ya kashfa yenyewe au kutokana na mambo mengine yasiyofungamana na hayo maelezo ya kashfa au kutokana na baadhi ya maelezo hayo na ya mambo hayo mengine.

Ufanunuzi wa utangazaji usio halali

31. Kwa madhumuni ya sehemu hii ya Sheria hii, utangazaji wa mambo yenye kashfa utahesabika kuwa si halali, isipokuwa kama:-

(a) mambo yenyewe ni ya kweli na yanatangazwa kwa manufaa ya Umma;

(b) utangazaji wa mambo hayo umehalalishwa na mojawapo ya masharti yaliyoelezwa ndani ya Sheria hii.

Utangazaji wa

32.-(1) Utangazaji wa mambo yenye kashfa utahesabika kuwa

mambo yenye
kashfa ambayo
ni halali

ni halali kabisa na hapana mtu yeyote anayeweza kuadhibiwa chini ya Sheria hii, ikiwa:-

- (a) mambo hayo yanatangazwa na Rais, Serikali au Bunge katika hati au shughuli yoyote ya kiserikali;
- (b) mambo hayo yanatangazwa katika Bunge na Rais, Serikali , Mjumbe yeyote wa Bunge au Spika;
- (c) mambo hayo yanatangazwa kwa amri ya Rais au Serikali;
- (d) mambo hayo yanatangazwa kuhusu mtu yeyote ambaye anatakiwa kufuata Sheria na Kanuni za Kikosi cha Wanamaji au kikosi kingine chochote cha Jeshi la Ulinzi la Nchi na mambo hayo yametangazwa kuhusu tabia ya mtu kama huyo na yanatangazwa na mtu yeyote aliye na mamlaka juu ya huyo Mwanajeshi kuhusu tabia hiyo;
- (e) mambo hayo yanatangazwa wakati wa kusikilizwa kwa shauri lolote Mahakamani na yanatangazwa na mtu anayeshiriki katika shauri hilo kama Jaji, Hakimu, Kamishna, Wakili, Mzee wa Baraza, Shaidi au Muhusika yeyote.
- (f) Mambo hayo yanayangazwa ni taarifa ya kweli na sahihi ya jambo lolote lililosemwa, lililoundwa au lililotangazwa katika Bunge ;au
- (g) Mtu huyo anayangaza mambo hayo ana jukumu, kwa mujibu wa Sheria, la kutangaza mambo hayo.

(2) Ikiwa utangazaji wa mambo yenye kashfa unahesabika kuwa ni halali, basi kwa madhumuni ya sehemu hii ya Sheria hii, siyo muhimu kama mambo hayo ni ya kweli au ya uongo, na kama inajulikana au haijajulikani au haisadikiwi kwa mambo hayo ni ya kweli au ya uongo na kama yametangazwa kwa nia safi au sivyo.

Hakuna jambo lolote katika fungu hili litakalo msalimisha mtu yeyote na jukumu la kuadhibiwa kwa mujibu wa Sheria nyingine yoyote kwa makosa ya madai au ya jinai, ikiwa utangazaji wa jambo husika umezuiliwa au unafuu wa mtu aliyeathirika umetajwa katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano.

Utangazaji wa
mambo yenye
Kashfa si halali

33. Utangazaji wa mambo yenye kashfa utahesabika kuwa ni halali kwa masharti maalumu ikiwa mambo hayo yanatangazwa kwa

ila kwa Masharti
Maalum

nia safi na ikiwa uhusiano baina ya mtu anayetangaza na mtu anayetangaziwa mambo hayo unamfanya mtu huyo mtangazaji kuwa na jukumu la kumtangazia huyo mtu mwingine ama kwa mujibu wa Sheria au kufuatana na mila au kanuni za mwenendo bora katika jamii kwa jumla au ikiwa huyo mtangazaji anatekeleza maslahi yake yaliyo halali kwa kutangaza mambo hayo; ila kwa sharti kwamba katika hali kama hiyo huo utangazaji hauzidi mpaka kwa namna yoyote, na pia utangazaji utahesabika kuwa ni halali kwa masharti maalumu kwa mujibu wa masharti yafuatayo, yaani ikiwa;

- (a) mambo yanayotangazwa ni taarifa ya kweli na sahihi ya jambo lolote lililosemwa, lililotendwa au lililoonekana katika shauri lolote la madai au la jinai linalosikilizwa mahakamani; isipokuwa kwamba iwapo mahakama itapiga marufuku utangazaji wa jambo lolote lililosemwa au lililoonekana katika mahakama hiyo kwa sababu kwamba jambo hilo huchochea uasi, ni ovu au ni la kukufuru basi utangazaji wa jambo kama hilo hautahesabika kuwa ni halali;
- (b) mambo yanayotangazwa yametokana na nakala au muhtasari halisi wa mambo yaliyopata kutangazwa wakati uliopita, na ikiwa utangazaji wa mambo hayo wakati uliopita ulikuwa halali, kwa mujibu wa sehemu hii ya sheria hii;
- (c) mambo hayo ni maoni yaliyotolewa kwa nia safi kuhusu vitendo vya kikazi vya mtu yeyote mwenye madaraka katika shughuli za mahakama, kiofisi au majukumu ya umma, au tabia yake binafsi kwa kadri tabia hiyo inavyoonekana katika vitendo vya kikazi;
- (d) mambo hayo ni maoni yaliyotolewa kwa nia safi kuhusu vitendo vya mtu yeyote vinavyohusika na suala la jambo lolote linalohusu umma, au kuhusu tabia yake binafsi kwa kadri tabia hiyo inavyoonekana katika vitendo kama hivyo;
- (e) mambo hayo ni maoni yaliyotolewa kwa nia safi juu ya tabia ya mtu yeyote kama ilivyoonekana kwenye ushahidi uliotolewa katika shauri lolote la kisheria lililosikilizwa hadharani, kama ni shauri la madai au la jinai kuhusu tabia ya mtu yeyote ambaye katika shauri hilo anashiriki kama

- mshtaki au mshtakiwa, mdai au mdaiwa, shahidi au anashiriki kwa namna nyingine yoyote, au kuhusu tabia binafsi kwa kadri tabia hiyo inavyoonekana kwa jinsi ilivyoelezwa katika fasili hii;
- (f) mambo hayo ni maoni yaliyotolewa kwa nia safi kuhusu ubora wa kitabu chochote, maandishi, picha au mchoro, hotuba au shughuli nyingineyo yoyote, maonesho au tendo lililotangazwa au kutendwa kwa hadhara au lililotendwa au kutolewa hadharani kwa ajili ya kutaka kupata maoni ya watu, au kuhusu tabia binafsi ya mtu yoyote anayehusika na lolote kati ya mambo hayo yaliyotajwa kwa kadri tabia hiyo inavyoonekana katika mambo hayo;
 - (g) mambo hayo ni lawama iliyotolewa na mtu kwa nia safi kuhusu vitendo vya mtu mwingine katika jambo lolote ambalo huyo aliyetoa lawama ana mamlaka nalo, ama kwa mujibu wa mkataba au vinginevyo na kwa kadri anavyohusika huyo aliyelaumiwa au kuhusu tabia binafsi ya mtu huyo aliyelaumiwa kwa kadri tabia hiyo inavyoonekana katika vitendo hivyo;
 - (h) mambo hayo ni malalamiko au mashtaka yaliyotolewa na mtu kwa nia safi dhidi ya mtu mwingine kuhusu vitendo vya mtu huyo mwingine katika jambo lolote, au kuhusu tabia yake binafsi kwa kadri tabia hiyo inavyoonekana katika vitendo hivyo, na ikiwa malalamiko au mashtaka hayo yametolewa mbele ya mtu ambaye ana mamlaka, ama kwa mujibu wa mkataba au vinginevyo juu ya mtu huyo aliyelaumiwa au kushtakiwa kuhusu vitendo vyake au tabia yake, au malalamiko au mashtaka hayo yametolewa mbele ya mtu ambaye kwa mujibu wa sheria ana mamlaka ya kuchunguza au kupokea malalamiko yanayohusika na vitendo au tabia kama hiyo; au
 - (i) mambo hayo yanatangazwa kwa nia safi kwa ajili ya kulinda haki au maslahi ya mtu huyo anayetangaza mambo hayo, au haki au maslahi ya mtu anayetangaziwa mambo hayo.

Nia ya kufanya
Marekebisho

34.-(1) Mtu atakayetangaza jambo linalodhaniwa ni la kashfa

kwa mtu mwingine anaweza, kama atadai kuwa jambo hili alilitangaza kwa nia safi kuhusu mtu huyo, ataonesha nia ya kufanya marekebisho kuhusu kashfa husika na katika jambo hilo; kama:

- (a) marekebisho yatakubaliwa na mtu aliyeathirika na kurekebishwa kikamilifu hakutakuwa na mashtaka ya kashfa dhidi ya mtu aliyefanya marekebisho juu ya kashfa husika, lakini bila kuathiri hatua yoyote dhidi ya mtu mwingine anayewajibika kwa pamoja na utangazaji huo;
 - (b) marekebisho hayatakubaliwa na aliyeathirika, isipokuwa imeelezwa vinginevyo na kijifungu hiki, itakuwa ni utetezi kwa mtu aliyefanya marekebisho husika katika shauri lolote la upande ulioathirika na kashfa dhidi ya mtu aliyefanya marekebisho kuhusu utangazaji wa kashfa husika kuthibitisha kwamba:
 - (i) jambo linalolalamikiwa lilitangazwa na upande wa utetezi kwa nia safi kuhusiana na mlalamikaji; au
 - (ii) Marekebisho yalifanywa mara tu baada ya upande wa utetezi kupokea taarifa kuwa kunaweza kukawa na kashfa dhidi ya mlalamikaji; na haijaondolewa.
- (2) Marekebisho yaliyofanyika kwa mujibu wa kifungu hiki yataambatanishwa na Hati ya Kiapo ikielezea hoja kwamba jambo linalohesabika kuwa ni kashfa lilitangazwa kwa nia safi kuhusiana na mlalamikaji.
- (3) Kwa madhumuni ya utetezi chini ya aya ya (b) ya kifungu kidogo cha (1), hakuna ushahidi zaidi ya hoja zilizotolewa katika hati ya kiapo, ambao utakubalika kwa niaba ya mtu aliyefanya marekebisho kuthibitisha kuwa jambo hilo lilitangazwa.
- (4) Nia ya kufanya marekebisho inayoelezwa itatafsiriwa na kueleweka kuwa-
- (a) kwa vyovyote vile, kutangaza au kuunganisha utangazaji wa usahihi wa maneno yanayolalamikiwa na kuomba radhi kikamilifu kwa mtu aliyeathirika na maneno husika;
 - (b) ambapo nakala ya nyaraka au kumbukumbu yenye maneno imesambazwa au kwa uelewa wa mtu wa anayefanya marekebisho, kuchukua hatua kwa namna ambayo inafaa kwa kuwajulisha watu ambao wamesambaziwa nakala zenye

maneno yenye kashfa dhidi ya mlalamikaji.

(5) Ambapo nia ya kufanya marekebisho imekubaliwa na mlalamikaji:-

- (a) jambo lolote katika kuchukua hatua zinazotakiwa katika kufanya marekebisho, kama zilivyokubaliwa na pande husika, ikitokea kutokubaliana na pande husika, jambo hili litaamuliwa na Mahakama ambapo uamuzi wake utakuwa wa mwisho;
- (b) mamlaka ya Mahakama kuamuru kuhusu gharama za uendeshaji wa shauri dhidi ya upande wa aliyefanya marekebisho kuhusu utangazaji husika au uendeshaji wa shauri unaohusiana na nia inayoelezwa katika fasili (a) itajumuisha mamlaka ya kumuamuru anayefanya marekebisho kumlipa mlalamikaji fidia na gharama zilizohusika au zilizotumika na mhusika kuhusiana na utangazaji husika.

(6) Ambapo hakuna mashtaka yaliyofunguliwa kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (1) Mahakama inaweza, kutokana na maombi ya mlalamikaji kuamuru kulipa gharama kadri Mahakama itakavyoona kuwa ni halali na inafaa.

(7) Kwa madhumuni ya kifungu hiki, maneno yatachukuliwa kuwa yametangazwa na mtu, katika kifungu hiki atajulikana kama mtangazaji, kwa nia safi kuhusiana na mtu mwingine ikiwa masharti yafuatayo yatazingatiwa.

- (a) mtangazaji hakuwa na nia ya kutangaza maneno kuhusiana na mtu mwingine, na hakujua mazingira ya namna ambayo ingeeleweka na mtu mwingine;
- (b) maneno hayakuwa ya kashfa kwa kuyatazama na mtangazaji hakujua mazingira ya namna ambayo ingeeleweka na mtu mwingine kuwa ni kashfa na katika namna yoyote mtangazaji alichukua tahadhari kuhusiana na utangazaji husika;

(8) Marejeo yoyote katika kifungu kidogo cha (7) kwa mtangazaji yatafikiriwa kuhusisha mtumishi au mwakilishi wa mtangazaji aliyehusika na maudhui ya tangazo.

(9) Matakwa ya fasili (b) ya kifungu kidogo cha (1)

hayatamhusu mtangazaji wa maneno ambaye siyo mwandishi mpaka pale atakapothibitisha kuwa maneno yaliyotangazwa yaliandikwa na mwandishi bila nia ovu.

Malalamiko
dhidi ya kashfa

35.-(1) Pale mtu anapodai kuwa maudhui ya chapisho au tangazo ni ya kashfa kwa maana ya sheria hii, mtu huyo aweza kuwasilisha malalamiko yake katika Bodi kwa usuluhishi.

(2) Malalamiko yatakuwa na nakala ya chapisho au tangazo lenye maudhui yanayolalamikiwa au kama maudhui ya chapisho au tangazo hayawezi kupatikana kwa namna yoyote, maelezo ya kutopatikana kwa maudhui husika.

(3) Baada ya kupokea malalamiko, Bodi itasikiliza malalamiko husika na pale itakapona inafaa kuwaita wahusika kwa ajili kuthibitisha au kutokuthibitisha malalamiko hayo.

(4) Bodi itafanya uamuzi kuhusu malalamiko kwa haraka na litaandaa na kuwasilisha taarifa kwa Waziri.

(5) Mtu ambaye hataridhika na uamuzi wa Bodi anaweza kukata rufaa Mahakamani.

SEHEMU YA NANE MAKOSA MBALIMBALI

Makosa
yanayohusu
vyombo vya
habari

36. Mtu yeyote atakayetumia kwa namna yoyote huduma ya habari kwa madhumuni ya kutangaza-

(a) kwa makusudi au kwa uzembe habari za uongo kwa namna ambayo-

(i) zitahatarisha Ulinzi, Usalama wa Umma, Utulivu wa Umma na maslahi ya kiuchumi ya Jamhuri ya Muungano, misingi ya maadili au masuala ya afya kwa umma; au

(ii) zitaharibu sifa, haki na uhuru wa watu wengine.

(b) taarifa yenye nia ovu au ya kutungwa na ya uongo;

(c) Tamko lolote lenye maudhui ambayo:-

(i) yatahatarisha Ulinzi, Usalama wa Umma, Utulivu wa Umma na maslahi ya kiuchumi ya nchi, misingi ya maadili au masuala ya afya kwa umma; au

- (ii) yataharibu sifa, haki na uhuru wa watu wengine.
- (d) kwa kujua kuwa tamko ni la uongo na bila sababu za kuamini kuwa ni kweli;
- (e) kwa uzembe au kwa nia ovu au kwa uongo kuwasilisha tamko kama tamko la kweli;
- (f) kutumia Chombo cha Habari bila kusajili;
- (g) bila kuwa na ithibati;
- (h) kwa kusambaza taarifa za uongo isivyo halali:
 - (i) kwa kuchapisha, kuuza, kuonyesha nia ya kuuza, kusambaza au kudurufu taarifa za uchochezi;
 - (ii) kwa kuwa na habari zilizokatazwa.

atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia mbele ya Mahakama atapaswa kuadhibiwa kwa kutozwa faini isiyopungua shilingi milioni ishirini au kufungwa gerezani kwa muda sio chini ya miaka mitano au kupewa adhabu zote mbili pamoja.

Makosa dhidi ya utangazaji

37.-(1) Mtu yeyote atakayeingiza nchini, atakayetangaza, atakayeza, atakayegawa au atakayetengeneza tangazo lolote ambalo uingizaji wake umepigwa marufuku atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia mbele ya Mahakama atapaswa kuadhibiwa, kwa kosa la kwanza faini isiyopungua shilingi milioni tano au kifungo kisichopungua miaka mitatu au vyote kwa pamoja na kwa kosa jingine lolote milioni nane au kufungwa gerezani muda usiopungua miaka mitano.

(2) Mahakama inaweza kuamuru kutaifishwa kwa tangazo au sehemu inayohusika na utendaji wa kosa.

Nia ya kuchochea uasi

- 38.**-(1) Nia ya kuchochea uasi ni nia ya:
- (a) kuchochea chuki au ufidhuli au uasi dhidi ya Jamhuri ya Muungano au Serikali yake;
 - (b) kuchochea wakazi wote wa Jamhuri ya Muungano kujaribu kuleta mapinduzi ya kijambazi ya jambo lolote katika Jamhuri ya Muungano liliowekwa kwa Mujibu wa Sheria;
 - (c) kuchochea chuki au ufidhuli au uasi dhidi ya utekelezaji wa haki katika Jamhuri ya Muungano;
 - (d) kuchochea manung'uniko na chuki au uasi miongoni mwa

- wakazi wa Jamhuri ya Muungano; au
- (e) Kuchochea uhasama baina ya vikundi mbalimbali vya wakazi wa Jamhuri ya Muungano.
- (2) Kitendo, hotuba au tangazo halitahesabika kuwa ni la kuchochea uasi ikiwa lengo lake ni-
- (a) kuonyesha kwamba Serikali imepotoshwa au imekosea katika shughuli yake yoyote; au
- (b) kuonyesha makosa au hitilafu katika Serikali au Katiba ya Jamhuri ya Muungano au katika Sheria za nchi au katika utekelezaji wa haki, kwa madhumuni ya kusahihisha au kurekebisha makosa hayo au hitilafu hizo.
- (3) Katika kufikiria kama jambo lolote lilitendwa, maneno yoyote yalitamkwa au hati yoyote iliyochapishwa na kutangazwa kwa nia ya kuchochea uasi, kila mtu atahesabika kuwa ana jukumu kamili juu ya matokeo yote ya vitendo vyake vyote vya makusudi.

Makosa ya
uchochezi

- 39.**-(1) Mtu yeyote ambaye-
- (a) atatenda au kujaribu kutenda, au atatayarisha kutenda, au atakula njama na mtu yeyote kutenda jambo lolote kwa nia ya kuchochea uasi;
- (b) atatamka maneno yoyote kwa nia ya kuchochea uasi;
- (c) atachapisha, kutoa, kuuza, kuchuuza, kugawa au kutengeneza nakala ya tangazo linalochochea uasi;
- (d) ataingiza nchini tangazo la uchochezi isipokuwa kama hana sababu ya kuamini kwamba tangazo hilo linachochea uasi; atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia mbele ya Mahakama atapaswa kuadhibiwa kwa kosa la kwanza kutozwa faini sio chini ya shilingi Milioni tano au kufungwa gerezeni kwa muda usiopungua miaka mitatu au kupewa adhabu zote mbili pamoja, na kwa kosa jingine lolote kutozwa faini isiyopungua shilingi Milioni saba au kufungwa gerezeni kwa muda usiopungua miaka mitano au kupewa adhabu zote mbili pamoja.
- (2) Mtu yeyote bila kuwa na sababu inayokubalika kisheria, atakuwa na tangazo linalochochea uasi; atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia mbele ya Mahakama atapaswa kuadhibiwa kwa

kosa la kwanza kwa kutozwa faini isiyopungua shilingi Milioni mbili au kufungwa gerezani kwa muda wa miaka miwili au kupewa adhabu zote mbili pamoja, na kwa kosa jingine lolote kwa kutozwa faini isiyopungua Shilingi Milioni tatu au kufungwa gerezani miaka mitatu au kupewa adhabu miaka zote mbili pamoja.

(3) Endapo mtu atashitakiwa kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (2) basi Mahakama itabidi ikubali kuwa kuna utetezi wa kutosha ikiwa wakati alipopata hilo tangazo huyo Mshtakiwa hakujua kwamba tangazo hilo lilichochea uasi na kwamba mara tu alipogundua yaliyokuwamo katika tangazo hilo alilipeleka kwa ofisa utawala aliyekuwa karibu naye au kwa Mkuu wa Kituo cha Polisi kilicho karibu naye.

(4) Mashine ya kupigia chapa yoyote iliyotumiwa au inayotuhumiwa imetumika kwa ajili ya kupigia chapa au kutengeneza nakala ya tangazo linalochochea uasi yaweza kuchukuliwa au kuzuiliwa na Ofisa wa Polisi wakati wa kungojea kusikilizwa shauri na kutolewa hukumu juu ya mtu yeyote aliyeshitakiwa kwa kosa la kuchapisha au kutengeneza nakala ya tangazo linalochochea uasi.

(5) Iwapo mtu yeyote atapatikana na hatia ya kuchapisha au kutengeneza tangazo linalochochea uasi, Mahakama yaweza, pamoja na adhabu nyingine yoyote inayoweza kumpa mshitakiwa, kuamuru kwamba hiyo mashine iliyotumika kwa ajili ya kupigia chapa au kutengeneza hilo tangazo linalochochea uasi, ama ichukuliwe na Serikali kwa muda usiozidi miezi kumi na mbili au ichukuliwe kabisa na Serikali na Mahakama hiyo yaweza kutoa amri kama hiyo hata kama hiyo mashine iliyotumika haikuwa mali ya huyo mshitakiwa.

(6) Mashine ya kupigia chapa iliyochukuliwa na Serikali kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (5) itauzwa na fedha itakayopatikana itapelekwa kwenye Mfuko wa Huduma za Habari.

(7) Endapo mmiliki, mtangazaji, mchapishaji, au mhariri wa gazeti atapatikana na hatia kwa kosa la kuchapisha gazeti au kutoa tangazo linalochochea uasi, hiyo mahakama yaweza pamoja na adhabu nyingine yoyote inayoweza kumpa mshitakiwa, itatoa amri yoyote kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (5) au sivyo kutoa amri ya kupiga marufuku uchapishaji wa tangazo hilo kwa muda usiozidi miezi kumi na mbili.

(8) Kabla Mahakama haijatoa amri kwa mashine ya kupigia chapa au kutangazia kuchukuliwa na Serikali kwa mujibu wa fungu hili, itabidi iridhike kwamba mashine hiyo ndiyo iliyotumika kwa ajili ya kupigia chapa gazeti au kutangazia tangazo hilo linalochochea uasi;

(9) Iwapo mashine ya kupigia chapa au kutangazia imechukuliwa na Serikali au na Mkuu wa Jeshi la Polisi kwa nadhari yake aweza:

(a) kuagiza kwamba hiyo mashine yote au sehemu yoyote ya mashine hiyo iondolewe;

(b) kuagiza kwamba sehemu fulani ya mashine hiyo izibwe au ifungwe ili kuzuia isitumike.

(10) Mkuu wa Jeshi la Polisi wakati akitekeleza madaraka yake kwa mujibu wa fungu hili hatakuwa na lawama kwa ajili ya hasara yoyote itakayotokea inayohusika na mashine hiyo, iwe hasara hiyo imesababishwa na uzembe au kwa namna nyingine yoyote.

(11) Mtu yeyote atakayetumia au kujaribu kutumia mashine ya kupigia chapa iliyochukuliwa na Serikali kwa mujibu wa kifungu cha (4) atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia mbele ya mahakama atapaswa kuadhibiwa kwa kutozwa faini isiyopungua shilingi milioni kumi na tano au kufungwa gerezani kwa muda usiopungua miaka mitatu au kupewa adhabu zote mbili pamoja.

Utangazaji wa habari za uongo za kutia hofu na woga kwa jamii

40.-(1) Mtu yeyote atakayetengeneza au kueneza habari yoyote ya uongo, uzushi au taarifa ambayo yaweza kuwatia watu woga na wasiwasi au kuchafua amani katika nchi atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia mbele ya mahakama atapaswa kuadhibiwa kwa kutozwa faini isiyopungua shilingi milioni kumi na tano au kufungwa gerezani kwa muda usiopungua miaka mitatu au kupewa adhabu zote mbili pamoja.

(2) Iwapo mtu yeyote atashtakiwa kwa kosa chini ya kifungu kidogo cha (1), Mahakama itabidi ikubali kuwa kuna utetezi wa kutosha ikiwa mshtakiwa atathibitisha kwamba kabla ya kutangaza au kueneza habari au taarifa ya aina iliyoelezwa katika kifungu kidogo cha (1) alichukua hatua madhubuti za kuhakikisha ukweli wa mambo na kwamba matokeo yake yalimfanya asadiki kwamba habari au taarifa hiyo ilikuwa ya kweli.

Makosa
yanayotendwa
na Mashirika ya
Vyama

41.-(1) Iwapo kosa lolote chini ya sheria hii litatendwa na kampuni, au shirika jingine lolote au na chama, umoja au kikundi cha watu basi pamoja na kampuni hiyo au shirika hilo jingine, au chama, umoja au kikundi cha watu kila mtu ambaye wakati wa kosa hilo lilipotendeka alishiriki au kuhusika, kama Mkurugenzi au Ofisa katika uongozi au uendeshaji wa kazi na shughuli za hiyo kampuni au shirika jingine au chama, umoja au kikundi cha watu, atakuwa ametenda kosa na atapaswa, akipatikana na hatia kupewa adhabu ya kulipa faini isiyopungua shilingi milioni kumi na tano.

(2) Iwapo mtu yeyote atashtakiwa, Mahakama itabidi ikubali utetezi wa kutosha ikiwa mshtakiwa atathibitisha kwamba hakujua na wala asingeweza kutumia hekima yoyote kujua kwamba kosa limetendeka.

Dhima ya
Mwajiri au mtu
anayemwakilisha

42. Iwapo kosa lolote chini ya Sheria hii litatendwa na mtu yeyote ambaye ni mwakilishi au mtumishi wa mtu mwingine, basi pamoja na huyo mwakilishi au mtumishi, huyo mtu aliyewakilisha madaraka yake au huyo mwajiri atakuwa vilevile ametenda kosa hilo na atapaswa, akipatikana na hatia kuadhibiwa kwa kutozwa faini isiyopungua shilingi milioni kumi na tano isipokuwa kama ataithibitishia Mahakama kwamba hakujua wala asingeweza kutumia hekima yoyote kumwezesha kutambua utendaji wa kosa hilo.

SEHEMU YA TISA MASHARTI YA JUMLA

Uwezo wa
kupiga
marufumu
uingizaji wa
machapisho

43. Iwapo Bodi itaona kwamba uingizaji nchini wa chapisho lolote ni kinyume cha manufaa ya Umma, inaweza kwa nadhari yake, kutoa amri ya kupiga marufuku uingizaji nchini wa chapisho hilo na kutangaza katika gazeti la Serikali.

Mamlaka ya
kukamata

44. Mkurugenzi wa Huduma za Habari, afisa wa polisi au afisa yeyote aliyeidhinishwa anaweza, ikiwa ana sababu za msingi na kuamini kuwa chombo cha habari kimeanzishwa, kimesimikwa, kinaendeshwa kinyume na matakwa ya sheria hii, kukamata kifaa

chochote ambacho kinatumika au kitatumika kwa malengo hayo.

Utoaji wa taarifa

45.-(1) Ikiwa amri au maelekezo yoyote yatatolewa na Bodi kwa mujibu wa sheria hii hayatalazimika kutangazwa katika Gazeti la Serikali; amri au maelekezo hayo yatawasilishwa kwa kuwajulisha wahusika watakaoathirika na amri hiyo au maelekezo hayo kwa namna itakavyoamriwa na Waziri au Bodi.

(2) Kama amri au maelekezo yatatangazwa katika Gazeti la Serikali, watu wote wanaohusika watahesabiwa kuwa wana taarifa husika.

Bima

46.-(1) Kila mwajiri kwa mujibu wa Sheria hii atatakiwa kuweka kinga ya Bima kwa kila mtu aliyeajiriwa katika chombo cha habari husika.

(2) Kila Mwanahabari wa kujitegemea atapaswa kujiwekea kinga ya Bima kwa mujibu wa sheria hii.

Upatikanaji wa huduma za habarai

47.-(1) Mtoa huduma ya habari yeyote atahakikisha huduma yake inafikiwa na watu wenye ulemavu;

(2) katika kuhakikisha kwamba huduma ya habari inafikika, mtoa huduma ya habari atahakikisha uwepo wa lugha za alama na maandishi.

Kuzuia wajumbe wa Baraza kutekeleza majukumu

48.-(1) Mtu ambaye-

(a) bila ya kuwa na sababu atashindwa au kukataa kutii maelekezo halali ya Baraza;

(b) atazuia Baraza kutekeleza majukumu yake chini ya sheria hii;

(c) atatoa taarifa ambazo anajua kuwa sio sahihi au za kupotosha;

(d) akiwa mbele ya Baraza, atatoa maelezo ambayo anajua sio ya kweli,

atakuwa ametenda kosa.

(2) Mtu ambaye atakuwa amehukumiwa kutenda kosa chini ya kifungu hiki atalazimika kulipa fani ya shilingi milioni tatu au kifungo kwa kipindi cha mwaka mmoja au vyote.

(3) Mtu ambaye atakuwa amehukumiwa kutenda kosa chini ya kifungu hiki ikiwa atatenda kosa lingine atalazimika kulipa fani ya shilingi milioni tano au kifungo kwa kipindi cha miaka mitatu.

Kanuni

49. Waziri aweza kutunga kanuni kwa ajili ya utekelezaji bora wa madhumuni ya sheria hii.

Kufutwa kwa sheria
Sura ya 229 ya
149

50. Sheria ya Magazeti na Sheria ya Shirika la Habari Tanzania zinafutwa.

Masharti ya mpito

49.-(1) Bila kujali utekelezaji wa sheria hii kuhusiana na sekta husika, kitambulisho chochote au cheti kilichotolewa, au leseni iliyotolewa kabla ya kuanza kutumika kwa sheria hii kuhusiana na uzalishaji, usambazaji au utoaji wa huduma za habari, zitaendelea kutumika mpaka zitakapofutwa, zitakapobatilishwa au kubadilishwa.

(2) Bila kujali kufutwa kwa Sheria ya Magazeti na Sheria ya Shirika la Habari Tanzania, watu wote wanaofanya kazi za Wanahabari bila sifa zilizoelzwa katika Sheria hii, watatakiwa ndani ya miaka mitano kukidhi masharti yaliyotolewa chini ya Sheria hii.

JEDWALI LA KWANZA

(Limetengenezwa chini ya kifungu cha 7)

MUDA, MWENENDO NA MASLAHI YA WAJUMBE WA BARAZA

- Muda wa uteuzi **1.**-(1) Mwenyekiti na Wajumbe wa Baraza watateuliwa kwa kipindi cha miaka mitatu na wanaweza wakateuliwa kwa kipindi kingine cha miaka mitatu.
(2) Utumishi wa Mwenyekiti na Wajumbe wa Baraza utasitishwa kwa sababu ya-
- (a) matumizi mabaya ya ofisi;
 - (b) rushwa;
 - (c) kushindwa kutekeleza majukumu
 - (d) kutokuwa na akili timamu; au
 - (e) matatizo yoyote ya kimwili au kiakili yatakayomfanya mtu asiweze kutekeleza majukumu ya ofisi husika; au
 - (f) kupatikana na hatia kwa makosa yanayohusu maadili; na
 - (g) kutangazwa kufilisika na Mahakama.
- (3) Mjumbe yeyote wa Baraza aweza kujiuzulu kwa kutoa taarifa ya mwezi mmoja ya maandishi kwa Waziri.
(4) Iwapo mjumbe yeyote hatahudhuria vikao vitatu vya Baraza mfululizo bila kutoa sababu za msingi Baraza itamshauri Waziri kutengua uteuzi wa mjumbe huyo na kuteua mjumbe mwingine kujaza nafasi hiyo.
- Kuhudhuria kwa wasio wajumbe **2.** Baraza yaweza kumualika mtu yeyote katika vikao vyake, kwa madhumuni ya kusaidia Baraza katika maamuzi yake, lakini mtu huyo hatakuwa na haki ya kupiga kura.
- Mikutano **3.**-(1) Mikutano ya Baraza itaitishwa na Mwenyekiti au akiwa hayupo au akiwa hajiwezi, Katibu atatoa taarifa ya mkutano ikiainisha tarehe, muda na mahali pa kufanyia mkutano.
(2) Taarifa itapelekwa kwa kila mjumbe katika eneo lake la kufanyia kazi, au makazi, si chini ya siku tano za kazi kabla ya tarehe ya kufanyika mkutano huo.
- Akidi **4.**-(1) Nusu ya Wajumbe wa Baraza itafanya akidi ya mkutano wa Bodi.
(2) Ikiwa Mwenyekiti hatakuwepo, wajumbe waliohudhuria mkutano huo wataamchagua mmoja kati yao kuwa Mwenyekiti wa mkutano huo.
(3) Katika mkutano wowote wa Baraza uamuzi wa wajumbe wengi waliohudhuria na kupiga kura utakubaliwa kuwa ni uamuzi wa Bodi; Hata hivyo mjumbe atakayekuwa tofauti na wajumbe walio wengi atakuwa na haki ya kuwa na uamuzi wake pamoja na sababu ambazo zitawekwa katika kumbukumbu za mkutano

huo.

- Kumbukumbu** **5.** Kumbukumbu za kila mkutano wa Baraza zitaandikwa na Katibu kwa namna inavyostahili na zitathibitishwa na Baraza na kusainiwa na Mwenyekiti na Katibu katika mkutano unaofuata wa Baraza.
- Taarifa ya Uamuzi** **6.** Taarifa ya uamuzi unaofanywa na Baraza na mawasiliano mengine yote yatasainiwa na Mwenyekiti au Katibu
- Taratibu za Uendeshaji** **7.** Kwa mujibu wa Sheria hii na maelekezo mengine yoyote kutoka kwa Waziri, Baraza yaweza kujiwekea taratibu za kujiendesha.
- Kamati ndogo** **8.** Bodi yaweza kuunda kamati ndogo mbalimbali na kuteua wajumbe wa kamati hizo, ambao wanaweza kuwa wajumbe wa Baraza au sio kwa madhumuni ya kuishauri Baraza katika jambo mahususi.
- Maslahi na Marupurupu** **9.** Wajumbe wa Baraza watalipwa mshahara na marupurupu kama Waziri atakavyoamua.

JEDWALI LA PILI

(Limetengenezwa chini ya kifungu cha 16(3))

Makamu
Mwenyekiti

1. Wajumbe wa Bodi watamchagua mjumbe mmoja miongoni mwao kuwa Makamu Mwenyekiti ambaye, kwa kuzingatia kuendelea kwa kipindi cha ujumbe wake, atakuwa makamu Mwenyekiti kwa kipindi kimoja cha mwaka mmoja na anaweza kushagulwika tena kwa kipindi kimoja.

Muda wa
uteuzi

2.-(1) Mjumbe wa Bodi atakuwa Ofisi kwa kipindi kingine kisichozidi miaka mitatu kuanzia siku aliyoteuliwa na anaweza kuteuliwa kwa kipindi kimoja.

(2) Kwa mjumbe ambaye ni mjumbe wake unatokana na ofisi, mjumbe huyo hatakuwa mjube pale ambapo atakoma kuwa mfanyakazi kwenye ofisi husika.

(3) Mjumbe yeyote anaweza, kujiuzuru wakati wowote kwa kuandikia mamlaka ya uteuzi.

(4) Bila kujali vifungu vya hapo juu, mamlaka ya uteuzi, wakati wowote inaweza kutengua uteuzi wa mjumbe.

(5) Pale ambapo mjumbe wa Bodi ambaye ni mjumbe kutokana na ofisi yake awezi kuudhuria vikao vya Bodi kwa sababu yoyote ili, mjumbe huyo anaweza, kumteua kwa maandishi mtu mwingine kutoka ofisini kwake kuudhuria, vikao vya Bodi kwa niaba yake.

(6) Pale ambapo kuna nafasi wazi ya mjumbe kwa sababu yoyote ili, Mamlaka ya uteuzi inaweza kumteua mtu mwingine kujaza nafasi hiyo na mtu huyo aliyeteuliwa atakaa ofisini kwa kipindi kilichobaki cha mjumbe aliyechukua nafasi yake.

Miutano ya
Bodi

3.-(1) Bodi itakutana kwa ajili ya masuala yake katika muda na sehemu ambayo Bodi itaamua, ila italazimika kukutana walau mara moja kila baada ya miezi mitatu.

(2) Mwenyekiti au asipokuwe, Makamu Mwenyekiti, ataongoza kila kikao cha Bodi na pale ambapo Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti hawapo, wajumbe waliopo watamteua mmoja wao kuongoza kikao.

(3) Mjumbe ambaye atashindwa kuudhuria vikao vitatu vya Bodi bila ruksa ya Mwenyekiti, atakoma kuwa mjumbe.

Taarifa ya
kikao

4. Katibu wa Bodi atatoa taarifa kwa kila mjumbe ya muda na mahali kikao kitafanyiwa na atatumza kumbukumbu za kila kikao cha Bodi.

Akidi

5. Akidi ya kila kikao cha bodi itakuwa nusu ya wajumbe wote.

Maamuzi ya Bodi

6.-(1) Kila jambo lililoadiliwa kwenye Kikao cha Bodi litaamuliwa kwa wingi wa kura za wajubme walioudhuria na kupiga kura na pale ambapo kura zimelingana, mtu anayeongoza kikao atakuwa na kura ya veto tofauti na kura yake ya kawaida.

(2) Bila kujali haya ya (1), uamuzi unaweza kufikiwa na Bodi bila ya Kikao kwa njia ya kuzungusha karatasi husika kwa wajumbe.

Bodi kuidhinisha kumbukumbu za vikao

7.-(1) Bodi itawezesha kuandaliwa na kutunzwa kumbukumbu zote za vikao vyake na kila kumbukumbu vya kikao itasoma na kuidhinishwa kwenye kikao kinachofuata na kusainiwa na mtu aliyeongoza kikao.

Nafasi wazi haiwezi kubatilisha vikao

8. Tendo au kikao chochote cha Bodi hakitabilishwa kwa sababu tu kulikuwa na nafasi wazi ya mjumbe.

Amri, maelekezo n.k

9. Maelekezo, amri, taarifa na nyaraka zingine zilizoandaliwa au kutolewa kwa niaba ya Bodi zitasainiwa na-

(a) Mwenyekiti;

(b) Mkurugenzi wa habari au afisa yeyote aliyeteuliwa na Bodi kwa ajili hiyo.

Bodi kusimamia vikao vyake

10. Kwa kuzingatia vifungu vya jedwali hili, Bodi itasimamia vikao vyake yenyewe.

MADHUMUNI NA SABABU

Muswada huu unapendekeza kutunga Sheria ya Huduma za Habari kwa madhumuni ya kuweka utaratibu wa kisheria katika tasnia ya habari, kuunda Bodi ya huduma za habari, kuunda mfuko wa huduma za habari, masuala ya kashfa, makosa yanayohusiana na utangazaji na masuala yanayohusiana na hayo.

Muswada huu umegawanyika katika Sehemu Tisa, Sehemu ya Kwanza inahusika na masharti ya awali, ambayo ni jina la sheria, tarehe ya kuanza kutumika, matumizi na ufafanuzi wa maneno yaliyotumika.

Sehemu ya Pili inahusika na uanzishwaji wa Baraza la Huduma za Habari, majukumu ya Baraza, mamlaka ya Baraza, muda, mwenendo na maslahi ya wajumbe wa Baraza, Mkurugenzi wa Huduma za habari, utaratibu wa kutoa leseni na taratibu za kuwasilisha malalamiko.

Sehemu ya Tatu inahusika na vyombo vya habari na taasisi ambapo imeelezwa aina ya vyombo vya habari na umiliki na majukumu ya vyombo vya habari.

Sehemu ya Nne inahusika na uanzishwaji wa Bodi ya ithibati kwa wanahabari, kitambulisho na orodha ya wanahabari.

Sehemu ya Tano inahusika na Idara ya Habari – MAELEZO na majukumu yake.

Sehemu ya Sita inahusika na Mfuko wa Huduma za Habari ambapo vyanzo vya fedha za mfuko, hesabu na ukaguzi wa hesabu za mfuko vimeelezwa.

Sehemu ya Saba inahusika na masuala ya kashfa ambapo kumeelezwa ufafanuzi wa utangazaji usio halali, utangazaji wa mambo yenye kashfa ambao ni halali, utangazaji wa mambo yenye kashfa kwa masharti maalum, nia ya kufanya marekebisho na malalamiko dhidi ya kashfa.

Sehemu ya Nane inahusu makosa mbalimbali ambapo kumeelezwa, makosa yanayohusu vyombo vya habari, makosa dhidi ya utangazaji, nia ya kuchochea uasi, makosa ya uchochezi, utangazaji wa habari za uongo za kutia hofu na woga kwa jamii, makosa yanayotendwa na mashirika au vyama na dhima ya mwajiri au mtu anayewakilisha.

Sehemu ya Tisa inahusika na mafungu ya jumla ambayo yameeleza uwezo wa kupiga marufuku uingizaji wa machapisho, mamlaka ya kukamata, utoaji wa taarifa, Bima, Kanuni, kufutwa kwa sheria na masuala ya mpito.

Dar es Salaam,
2 Februari, 2015

FENELLA E. MUKANGARA
Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo